Hojaji ya Uchunguzi wa Kabla ya Usajili

S#	Swali la Uchunguzi	Hatua ya Kuchukuliwa

1.	**Je, umewahi kuwa na athari mbaya ya mzio inayotishia maisha* (kama anaphylaxis) kwa dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech, au kwa viambato vyovyote vya chanjo (ambayo ni pamoja na polyethilini glikoli)?**
	AU
	Je, umewahi kuwa na athari ya mzio wa ukali wowote ndani ya saa 4 baada ya kupokea dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech au mzio uliogunduliwa kwa kiambato fulani kwenye chanjo (ikiwemo polyethilini glikoli)? (*Kumbuka: Athari za mzio zinaweza kujumuisha dalili kama vile ugonjwa wa mabaka ngozini; uvimbe wa uso, mdomo, au koo; au kukorota na kupumua kwa shida.*)
	
	Viambato vya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ni pamoja na:
	• Messenger RNA (mRNA)
	• Lipidi:
	  ○ ((4-hydroxybutyl)azanediyl)bis(hexane-6,1-diyl)bis(2-hexyldecanoate)
	  ○ 2[(polyethylene glycol)-2000]-N,N-ditetradecylacetamide
	  ○ 1,2-distearoyl-sn-glycero-3-phosphocholine
	  ○ Kolesteroli
	• Potasiamu kloridi
	• Potasiamu fostefi ya monobasic
	• Sodiamu kloridi
	• Sodiamu fosfeti dihaidreti ya dibasic
	• Sukrosi	

	➢ **NDIYO**	USIMPE chanjo ya Pfizer-BioNTech au Moderna. Mtu huyo anaweza kupewa chanjo ya Janssen ikiwa hakuna sababu ya kutopewa chanjo hiyo (angalia **Swali la 3** hapa chini), lakini mtu huyo lazima ajadili historia ya mzio na mtoa huduma wake wa msingi kwanza na afanyiwe tathmini ya kliniki. Chanjo ya Janssen inapaswa kuratibiwa kutolewa angalau siku 28 baada ya dozi yoyote ya awali ya chanjo ya Pfizer (ikiwa inafaa).
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #2

2.	**Je, umewahi kuwa na athari mbaya ya mzio inayotishia maisha* (kama anaphylaxis) kwa dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 ya Moderna, au kwa viambato vyovyote vya chanjo (ambayo ni pamoja na polyethilini glikoli)?**
	AU
	Je, umewahi kuwa na athari ya mzio wa ukali wowote ndani ya saa 4 baada ya kupokea dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 ya Moderna au mzio uliogunduliwa kwa kiambato fulani kwenye chanjo (ikiwemo polyethilini glikoli)? (*Kumbuka: Athari za mzio zinaweza kujumuisha dalili kama vile ugonjwa wa mabaka ngozini; uvimbe wa uso, mdomo, au koo; au kukorota na kupumua kwa shida.*)
	Viambato vya Chanjo ya Moderna ni pamoja na:
	• Messenger RNA (mRNA)
	• Lipidi:
	  ○ SM-102 (inahusiana na Moderna)
	  ○ Polyethylene glycol [PEG] 2000 dimyristoyl glycerol [DMG]
	  ○ 1,2-distearoyl-sn-glycero-3-phosphocholine [DSPC]	

	○ Cholesterol • Tromethamini • Tromethamini haidrokloridi • Asidi ya asetiki • Sodiamu asetati • Sukrosi

	➢ **NDIYO**	USIMPE chanjo ya Pfizer-BioNTech au Moderna. Mtu huyo anaweza kupewa chanjo ya Janssen ikiwa hakuna sababu ya kutopewa chanjo hiyo (angalia **Swali la 3** hapa chini), lakini mtu huyo lazima ajadili historia ya mzio na mtoa huduma wake wa msingi kwanza na afanyiwe tathmini ya kliniki. Chanjo ya Janssen inapaswa kuratibiwa kutolewa angalau siku 28 baada ya dozi yoyote ya awali ya chanjo ya Pfizer (ikiwa inafaa).
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #3
3.	**Je, umewahi kuwa na athari mbaya ya mzio inayotishia maisha* (kama anaphylaxis) kwa dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 ya Janssenau kwa viambato vyovyote vya chanjo (ambayo ni pamoja na polysorbate)?** **AU** **Je, umewahi kuwa na athari ya mzio wa ukali wowote ndani ya saa 4 baada ya kupokea dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19 ya Janssenau mzio uliogunduliwa kwa kiambato fulani kwenye chanjo (ikiwemo polysorbate)? (*Kumbuka: Athari za mzio zinaweza kujumuisha dalili kama vile ugonjwa wa mabaka ngozini; uvimbe wa uso, mdomo, au koo; au kukorota na kupumua kwa shida.*)** **Viambato vya Chanjo ya Janssen ni pamoja na:** • Chembe za adenovirus ambazo hazijaamilishwa • Monohaidrati ya aside ya sitriki • Dihaidrati ya trisodiamu sitrati • Ethanoli • 2-hydroxypropyl-β-cyclodextrin (HBCD) • Polysorbate-80 • Sodiamu kloridi	
	➢ **NDIYO**	Usimpe chanjo ya Janssen. Mtu huyo anaweza kupewa chanjo ya Pfizer au Moderna ikiwa hakuna sababu ya kutompa chanjo hizo (angalia **Maswali ya 1 na 2**), lakini mtu huyo lazima ajadili historia yake ya mzio na mtoa huduma wake wa msingi kwanza na afanyiwe tathmini ya kliniki.
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #4
4.	**Je, umewahi kuwa na athari mbaya ya mzio inayotishia maisha* (kama anaphylaxis) kwa chochote (ikiwemo dawa nyingine, chakula, dutu, hatari ya kimazingira, n.k.)?** **AU** **Je, umewahi kupata athari ya mzio wa ukali wowote ndani ya saa 4 baada ya kupokea chanjo nyingine au tiba ya kudungwa sindano (ikiwemo dawa za kudungwa sindano kwenye mshipa, misuli, au chini ya ngozi)?**	
	➢ **NDIYO**	Mtu huyo anaweza kuratibu chanjo, lakini pendekeza mtu huyo ajadili kwanza historia ya mzio, na hatari na faida za chanjo na mtoa huduma wa msingi. Mpe *"Taarifa kuhusu Chanjo ya COVID-19 kwa Watu walio na Hali Fulani za Kiafya"*. Wakati atapokea chanjo, atachunguzwa kwa dakika 30 baada ya kupewa chanjo.
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #5
5.	**Je, umepokea tiba ya kingamwili ya kutibu COVID-19 katika siku 90 zilizopita (hii ni pamoja na kinga ya mwili ya plasma na kingamwili za monoclonal, kama bamlanivimab na casirivimab/imdevimab)? (*Kumbuka: chanjo za COVID-19 hazipaswi kutolewa kwa angalau siku 90 baada ya mtu kupokea tiba ya kingamwili kama matibabu ya COVID-19 ili kuzuia uwezekano wa tiba ya kingamwili kuathiri chanjo.*)**	

	➢ **NDIYO**	USIRATIBU chanjo hadi siku 90 ziwe zimepita kutoka wakati wa tiba ya kingamwili.
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #6
6.	**Je, umepokea chanjo nyingine isiyohusiana (k.m., mafua) katika siku 14 zilizopita?** **(*Kumbuka: chanjo ya COVID-19 inapaswa kutolewa peke yake na angalau siku 14 tofauti na chanjo nyingine.*)** ➢ **Ikiwa Ndiyo, tarehe ya chanjo yako ya mwisho ya chanjo nyingine ni lini? (Weka Tarehe)**	
	➢ **NDIYO**	USIRATIBU chanjo hadi siku 14 ziwe zimepita kutoka wakati wa chanjo nyingine.
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #7
7.	**Je, kinga yako ya mwili ineathiriwa sana** (kinga yako imedhoofika na haifanyi kazi vizuri)?**	
	➢ **NDIYO**	Mtu huyo anaweza kuratibu chanjo, lakini pendekeza mtu huyo ajadili kwanza hali ya kinga, na hatari na faida za chanjo na mtoa huduma anayesimamia hali yake. Mpe *"Taarifa kuhusu Chanjo ya COVID-19 kwa Watu walio na Hali Fulani za Kiafya".*
	➢ **HAPANA**	Nenda kwa Swali #8
8.	**Je, una ujauzito kwa sasa?**	
	➢ **NDIYO**	Mtu huyo anaweza kuratibu chanjo, lakini pendekeza mtu huyo ajadili kwanza kuhusu ujauzito, na hatari na faida za chanjo na mtoa huduma wake wa uzazi. Mpe *"Taarifa kuhusu Chanjo ya COVID-19 kwa Watu walio na Hali Fulani za Kiafya".*
	➢ **HAPANA**	Mwisho

***** Athari kali za kutishia maisha ni pamoja na dalili za anaphylaxis kama vile uvimbe wa uso wako, mdomo, au koo; kukorota au kupumua kwa shida; kupoteza ghafla shinikizo la damu, nk. kawaida inahitaji mtu apewe epinephrine na aende hospitalini.

** Hali mbaya za kuathirika kwa kinga ni pamoja na kuwa kwenye kemotherapi ya saratani, kuwa ndani ya mwaka mmoja tangu ulipopokea seli ya hematopoietic au upandikizaji wa kiungo, maambukizo ya VVU yasiyotibiwa na hesabu ya CD4 ya lymphocyte ya chini ya 200, ugonjwa wa msingi wa upungufu wa kinga mwilini, viwango vya juu vya steroidi, na kadhalika